


MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA

Simu: +255-22-2133964, 2133969
Huduma kwa wateja: 0800 110063
Barua Pepe: info@nhif.or.tz
Tovuti: www.nhif.or.tz
Nukushi: +255-22-2133972,
2133982



Makao Makuu
Kurasini Bendera Tatu
S.L.P. 11360, Dar es Salaam
Tanzania

TAARIFA KWA UMMA

UFAFANUZI JUU YA SUALA LA WATEGEMEZI WA WANACHAMA WA NHIF, WANACHAMA WASTAAFU NA KUKATALIWA KWA KADI KATIKA VITUO VYA HUDUMA.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unapenda kufafanua juu ya taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii zikidai kuwa baadhi ya taratibu za Mfuko katika utoaji wa huduma zimelenga kuwaibia wanachama. Madai hayo sio ya kweli na Mfuko unapenda kufafanua taratibu sahihi zilizopo kwa lengo la kufanikisha utoaji wa huduma kwa wanachama wake kama ifuatavyo;-

1. Utaratibu wa wategemezi wa mwanachama mchangiaji

- i. Mwanachama mchangiaji ana nafasi ya kuwasajili mweza na wategemezi wake wanne. Mategemezi anaweza kuwa ni mtoto wa mwanachama, wazazi wake na wazazi wa mwenza wake.
- ii. Mwanachama anapowasajili wategemezi kwenye utaratibu huu atahitajika kuambatisha kithibitisho cha uhusiano kwa kila mategemezi anayemsajili. Mfano, kama atamjumuisha mtoto wake, atatakiwa kuambatisha nakala ya cheti cha mtoto cha kuzaliwa na kama ni mwenza, atatakiwa kuambatisha nakala ya cheti cha ndoa, ambapo kwa mzazi, cheti cha kuzaliwa cha mwanachama au mwenza wake kitaambatishwa.
- iii. Utaratibu huu unafanyika kwa lengo la kulinda uhai wa Mfuko kwa kudhibiti udanganyifu uliokuwa ukifanywa na baadhi ya wanachama wasio waaminifu kwa kuuza nafasi za wategemezi wao ili kujinufaisha.

2. Utaratibu wa huduma kwa Wanachama Wastaafu

- i. Tangu mwaka 2009, Mfuko uliweka utaratibu kwa mtumishi anayestaafu akiwa mwanachama mchangiaji wa NHIF kuendelea kunufaika na huduma za NHIF pamoja na mwenza wake kwa kipindi chote cha uhai wao bila kuendelea kuchangia.

- ii. Kunufaika kwa wategemezi wa mwanachama mstaafu kunakoma pale michango ya mwanachama huyu anayestaafu inakoma. Hivyo mwanachama mstaafu atatakiwa kurejesha vitambulisho vyote ambavyo alipewa awali na kuwasilisha barua ya kustaafu kwake ili aweze kunufaika na utaratibu huu.

3. Sababu za baadhi ya kadi kutotambuliwa katika vituo vya huduma

Kabla ya kupata huduma, mtoa huduma atahakiki kadi ya mwanachama kujua uhalali wake. Kutotambuliwa kwa baadhi ya kadi katika vituo vya kutolea huduma kunasababishwa na sababu zifuatazo;-

- Kutowasilishwa kwa michango ya mwanachama
- Mwanachama mchangiaji kumuondoa mtegemezi wake

Endapo kadi yako haitambuliki katika kituo ulichokwenda kupata huduma, tafadhali wasiliana na NHIF kupitia kituo cha huduma kwa wateja namba 0800 110063, au fika ofisi ya NHIF iliyo karibu nawe.

Mfuko unaendelea kuwajali wanachama wake kwa kuboresha huduma zake na kufuata taratibu ili kulinda uhai wa Mfuko huu kwa manufaa ya Watanzania wote na vizazi vijavyo.

Imetolewa na;

MKURUGENZI MKUU

FEBRUARI 15, 2018